**HOTUBA YA MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KUHUSU MATOKEO YA TAFITI YA HALI YA UZINGATIAJI MAADILI KATIKA UTUMISHI WA UMMA YA MWAKA 2022, KWENYE KIKAO KAZI CHA WADAU WA USIMAMIZI WA MAADILI KATIKA UTUMISHI WA UMMA KATIKA UKUMBI WA KAMBARAGE, DODOMA TAREHE 30 JANUARI, 2023**

***Dkt. Laurean J. P. Ndumbaro - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***

***Wakurugenzi wa OR - MUUUB;***

***Wakurugenzi wa Taasisi Simamizi za Maadili;***

***Wawakilishi wa Watendaji wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mahakama na Jeshi la Polisi Tanzania;***

***Mameneja na Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu;***

***Washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau;***

***Watumishi wa OR - MUUUB mliopo hapa;***

***Waandishi wa Habari mliopo hapa;***

***Mabibi na Mabwana.***

***"Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".***

***Ndugu Viongozi;*** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema tukijiandaa kupokea ***Matokeo ya Tafiti ya Hali ya Uadilifu katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2022***.

Kipekee nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa utayari wenu wa kushirikiana na Ofisi hii katika jukumu la kuimarisha masuala ya Kiutumishi na Utawala Bora kila inapohitajika. Hii inaonesha dhamira yenu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhakikisha tunakuwa na Utumishi wa Umma

wenye nidhamu, uwajibikaji wa hiari na utendaji wenye matokeo kwa ustawi wa Taifa letu.

***Ndugu Viongozi;*** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na majukumu mengine ya kusimamia Uendelezaji Sera katika Utumishi wa Umma, Utawala wa Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Mishahara, Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA ya Uendeshaji wa Serikali, Usimamizi wa Mifumo ya Utendaji Kazi wa kila Siku Serikalini, Uendelezaji Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Serikali Mtandao na Usimamizi wa Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma, **pia ina jukumu la *KUSIMAMIA MAADILI YA UTENDAJI KATIKA UTUMISHI WA UMMA NCHINI.***

***Ndugu Viongozi;*** Mtakumbuka kuwa mnamo mwezi Desemba 2022, tukiwa katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya ***Maadili na Haki za Binadamu*** kitaifa, moja ya mambo muhimu tuliyoyafanya OR MUUUB ilikuwa ni kutoa taarifa ya muhtasari wa matokeo ya "***Utafiti wa Hali ya Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma nchini kwa mwaka 2022" (Public Service Integrity Survey 2022)***. Utafiti huu ambao ulifanyika katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 uliongozwa na Mtaalam Mwelekezi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Kampasi ya Dar es Salaam kwa niaba ya OR MUUUB ili kuweza kupata maoni huru. Utafiti huu umefanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo hojaji.

***Ndugu Viongozi;*** Sote tunatambua kwamba Taasisi za Umma ndio msingi mkubwa wa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na mipango ya Serikali ya ***kukuza uchumi, kutoa huduma bora kwa jamii na kulinda amani na utulivu***.

Taasisi hizo zimeundwa kwa ajili ya kufanikisha jukumu la msingi la Serikali la kuleta ustawi kwa Wananchi. Hivyo, ni wajibu wa Taasisi za Umma nchini kuhakikisha zinafanikisha kufikiwa kwa malengo ambayo **Serikali imejiwekea Kitaifa na Kimataifa.**

Malengo hayo ambayo Serikali imejiwekea hayataweza kufikiwa endapo tutashindwa kuzingatia na kusimamia vyema Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma. Kwa kuzingatia hilo na dhamana ambayo nimepewa na Serikali ya Awamu ya Sita kusimamia masuala yote ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi yangu imekuwa ikitoa miongozo ya Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma; kuwajengea uelewa wa masuala ya Maadili ya Utendaji Watumishi wa Umma na Wananchi; na kufanya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Miongozo hiyo.

Utafiti ni moja ya njia zinazotumiwa na Ofisi yangu kutathmini Hali ya Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji ili kuiwezesha Serikali kufahamu hali ya Maadili katika Taasisi zake na kutumia mrejesho huo kutambua na kufanyia kazi maeneo ambayo yana kasoro/mapungufu ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

***Ndugu Viongozi;*** Tathmini ya Hali ya Uzingatiaji Maadili zinazofanyika katika Utumishi wa Umma zinalenga kupata taarifa sahihi za usimamizi wa ***Maadili ya Utendaji na Maadili ya Kitaaluma Katika Utumishi wa Umma***. Ili kuimarisha usimamizi wa Maadili katika Utumishi wa Umma, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi hii iliendesha Utafiti wa Hali ya Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2022 (Public Service Integrity Survey).

Lengo kuu ilikuwa ni **kubaini endapo kumekuwa na ongezeko la uzingatiaji wa viwango vya Maadili ya Utendaji kwa Watumishi Umma.**

***Ndugu Viongozi;*** Kama ambavyo nilizungumza wakati wa uzinduzi wa Tafiti hii, Tafiti ya kwanza ya Maadili (Integrity Survey) katika Utumishi wa Umma ilifanyika mwaka 2006 kwa lengo la kupata taarifa za msingi kwa ajili ya kuweka kiwango cha uzingatiaji wa Maadili (baseline information). Matokeo ya utafiti kwa mwaka 2005 yalionesha kuwa kiwango cha uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma kilikuwa asilimia 56.4 (56.4%). Kiwango hiki ndicho kilichukuliwa na kutumika kama "baseline" kwa kuwa awali hakukuwa na utafiti wowote ambao uliwahi kufanyika kupima hali ya uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma.

Mnamo mwaka 2014, ulifanyika utafiti mwingine ili kufahamu endapo kumekuwa na ongezeko la uzingatiaji wa viwango vya Maadili kwa Watumishi Umma; na kubaini maeneo yenye mianya ya uvunjifu wa Maadili kwa lengo la kuweka mikakati ya uimarishaji inayoendana na matokeo halisi. Kwa mwaka 2014 kiwango cha uzingatiaji wa Maadili kiliongezeka toka 56.4% (ya mwaka 2005) hadi kufikia asilimia 66.9 (66.9%).

***Ndugu Viongozi;*** Utafiti wa mwaka huu wa 2022 umefanyika baada ya kipindi cha miaka minane (8) kupita kutoka Tafiti ya mwisho iliyofanyika mwaka 2014. Lengo kuu la utafiti wa mwaka 2022 ilikuwa ni kubaini kama **kumekuwa na ongezeko la uzingatiaji wa viwango vya maadili katika Utumishi wa Umma** (follow up study) ambapo **Matokeo ya Utafiti wa Hali ya Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma kwa mwaka 2022 yameonesha kuwa kiwango cha**

**uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma kwa mwaka 2022 ni** asilimia 75.9 (**75.9%).** Matokeo haya yanaonesha kiwango cha uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma kimeongezeka kwa wastani wa asilimia 9.8 (9.8%) kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na 66.1% (ya mwaka 2014). Ongezeko hili la kiwango cha Maadili linatokana na dhamira ya uongozi thabiti wa Serikali Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu; Programu za mabadiliko ya Kisekta na Taasisi zenyewe; na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (NACSAP).

***Ndugu Viongozi;*** Kwa mujibu wa matokeo ya taarifa ya Utafiti huu, yapo maeneo ambayo bado yanahitaji kuboreshwa / kutiliwa mkazo. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Ufuatiliaji wa kila mara wa uzingatiaji wa kanuni za maadili kwa watumishi wa umma;

(ii) Mafunzo endelevu kwa watumishi ambao wako kazini; wale wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza na elimu kwa umma; na

(iii) Usimamizi wa uzingatiaji wa Maadili katika utoaji wa huduma wakati wa majanga ya kitaifa kama vile UVIKO-19 na majanga mengine mbalimbali yanayotokea nchini.

Aidha, maeneo ambayo yameonekana kulalamikiwa zaidi kutokana na kuwepo kwa viashiria vya kukithiri kwa vitendo visivyo vya uadilifu ni pamoja na Jeshi la Polisi; Mahakama; Manunuzi ya Umma, Mikataba; na Huduma za Ardhi. Matokeo kuhusu maeneo ambayo yamelalamikiwa zaidi kwa kiasi kikubwa yanashabihiana na matokeo yaliyotolewa katika utafiti wa kitaifa kuhusu Rushwa (National Governance and

Corruption Survey), utafiti ambao uliendeshwa na TAKUKURU mwaka 2020, ambapo utafiti huo pia ulibainisha kati ya Taasisi zinazolalamikiwa kuwa na viashiria vya kujihusisha na vitendo vya rushwa ni pamoja na Jeshi la Polisi; Mahakama; na Usimamizi wa Ardhi.

***Ndugu Viongozi; Tarehe 9 Desemba, 2022, wakati wa uzinduzi wa*** matokeo ya utafiti huu kwa Umma kupitia vyombo vya habari, nilitoa maelekezo katika maeneo sita ya kufanyiwa kazi. Eneo la kwanza ilikuwa ni kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya kikao kazi cha pamoja na wadau kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kina kuhusu matokeo ya utafiti huu na kuja na mikakati ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Maadili katika sekta zote kulingana na matokeo.

Katibu Mkuu (UTUMISHI) ametekeleza maagizo haya kwa kuandaaa mkutano huu kuhakikisha kuwa taarifa ya Utafiti huu inawafikia. Hivyo niwaelekeze kupokea taarifa hiyo ambayo itawasilishwa kwenu na Mtaalam Mwelekezi; kuchambua kwa kina taarifa hiyo; na kutoka na maazimio na mipango itakayowezesha Serikali kuboresha Usimamizi wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma.

Majadiliano yenu katika siku hizi mbili za kikao kazi yazingatie mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuweka mikakati ya kukuza Maadili inayoendana na hali halisi;

(ii) Kubaini maeneo yenye changamoto za kimaadili na kuishauri mamlaka ipasavyo;

(iii) kujitathmini kuhusu hali ya kimaadili ya Watumishi wa Umma na kushauri hatua stahiki

kwa maeneo ambayo yameonekana kuwa na mapungufu;

(iv) Kubaini maeneo ambayo yanafanya vizuri na kuweka mikakati ya kuendelea kujiimarisha; na

(v) Kuendelea kuimarisha dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika kuimarisha utendaji wa Serikali kama moja ya misingi ya Utawala Bora.

***Ndugu Viongozi;* kwa kuwa kikao kazi hiki kimeshirikisha Viongozi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia eneo la Maadili na Utawala Bora katika Taasisi zao, nitumie fursa hii kuwafahamisha maagizo mengine niliyoyatoa tarehe 9 Desemba 2022 wakati wa uzinduzi wa taarifa ya utafiti:-**

(i) Taasisi Simamizi za Maadili na Utawala Bora pamoja na Vyama vya Kitaaluma kuendelea kushirikiana na OR - MUUUB kukuza Maadili na

kutumia matokeo haya kuimarisha mikakati ya usimamizi katika maeneo yao;

(ii) Waajiri kuhakikisha wanatenga Bajeti ya mafunzo ya Maadili na kuendesha mafunzo kwa watumishi wa umma walio kazini na wale wanaoajiriwa. Kama ambavyo mmesikia moja ya eneo ambalo halikufanya vizuri ni eneo la mafunzo kwa watumishi;

(iii) Waajiri kuhakikisha wanaweka na kuimarisha mifumo ya utoaji wa mrejesho ndani ya Taasisi zao ili kuendelea kutoa fursa kwa wananchi kukemea vitendo vya ukiukwaji wa Maadili;

(iv) Waajiri kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo Vyombo vya Habari na Tovuti kuhusu haki na wajibu wa wananchi katika kupata huduma bora katika Taasisi za Umma; na

(v) Viongozi na Watumishi wa Umma wote nchini kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma kwa kuwa ndiyo nguzo kuu ya Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma.

***Ndugu Viongozi;*** Nichukue fursa hii tena kuwapongeza watumishi wa umma pamoja na Taasisi zote zilizofanya vizuri kwa mujibu wa utafiti huu, kwa kuweza kuzingatia na kuyaishi maadili ya utendaji katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Matarajio yangu ni kuwa washiriki wa mkutano huu, mtafanya uchambuzi wa kina wa taarifa hii na kutoka na maazimio ambayo yatasaidia kuimarisha hali ya uadilifu katika Utumishi wa Umma na hatimaye kuwa na Taasisi nyingi zaidi zinazofanya vizuri katika eneo la Maadili.

***Ndugu Viongozi; W*ashiriki wa kikao hiki na Waandishi wa Habari; ninapohitimisha hotuba yangu niwashukuru tena kwa kuendelea kuwa sehemu ya kufanikisha malengo ya Serikali na ushirikiano wenu** ambao mmekuwa mkiutoa pindi tunapowahitaji. Niwahakikishie kuwa Ofisi yangu itaendelea kufanya kazi nanyi bega kwa bega katika kuimarisha utendaji kazi kwenye Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

***Ndugu Viongozi na Washiriki wa kikao hiki;*** Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba ***KIKAO KAZI CHA WADAU KUPITIA NA KUJADILI RASIMU YA UTAFITI WA HALI YA UADILIFU KATIKA UTUMISHI WA UMMA*** umefunguliwa rasmi na ninawatakieni majadiliano mazuri yenye tija na ufanisi kwa ustawi wa Taifa letu.

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***

***KAZI IENDELEE***